**MAJUMUISHO YA ZIARA YA RAIS WA ZANZIBAR**
**NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**MHESHIMIWA DK. ALI MOHAMED SHEIN,**
**MKOA WA KUSINI UNGUJA KATIKA UKUMBI WA**
**ZANZIBAR UNIVERSITY, TUNGUU TAREHE 11 MACHI 2013**

## 1.0 UTANGULIZI:

Kwanza, tunawajibu wa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye wingi wa Rehma na Utukufu kwa kutuwezesha kukutana kwa mara nyengine katika ukumbi huu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar hapa Tunguu tukiwa katika hali ya uzima na salama. Pili, napenda kuushukuru kwa dhati uongozi wa Mkoa wa Kusini Unguja na Wilaya zake pamoja na watendaji kwa ratiba yenu iliyoniwezesha mimi na wenzangu kutembelea shughuli mbali mbali za maendeleo katika wilaya zote mbili, kusalimiana na wananchi na leo tupo katika siku ya pili ya ziara ambapo tunakamilisha ratiba yetu ya Mkoa wa Kusini Unguja kwa mkutano huu wa majumuisho.

Nachukua fursa hii kuwapongeza viongozi na wananchi kwa mafanikio niliyoyasikia kupitia taarifa niliyosomewa juzi pamoja na yale ambayo nimejionea mwenyewe katika ziara hiyo. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi kwa ushirikiano wao mkubwa kila tulipopita na kutupokea kwa shangwe na mahudhurio mazuri; katika kila kituo. Kwa niaba ya wenzangu nasema ahsanteni sana.

## 2.0 TAARIFA YA MKOA:

Kama kawaida nilianza ziara yangu kwa kupokea taarifa ya Mkoa, taarifa yenu imezidi kuwa bora ikilinganishwa na zile mbili zilizotangulia hali ambayo ni kielelezo cha kuzidi kusonga mbele. Taarifa imesomwa kwa umahiri na imeelezea taarifa za sekta mbali mbali zinazosimamiwa na Mkoa huu kwa kuzingatia majukumu, hali ya utendaji wa kila sekta na changamoto zilizopo. Baadhi ya mambo muhimu yaliokuwemo kwenye taarifa yenu ni pamoja na jiografia ya Mkoa, idadi ya wakaazi na muundo wa uongozi. Kwa mnasaba wa mkutano huu napenda nielezee baadhi ya mambo kuhusiana na taarifa yenu ya Mkoa.

2.1 **Ulinzi na Usalama:**

Nakupongezeni kwa taarifa yenu juu ya kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama katika mkoa wenu. Taarifa imeelezea kuwa matukio makubwa ambayo yalikua ni tishio na kero kwa wananchi yamedhibitiwa. Takwimu zinaonesha katika kipindi cha Juni hadi Disemba 2012 yameripotiwa makosa makubwa 686. Idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na makosa 1112 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2011 (yamepungua kwa asilimia 38). Hongereni sana kwa mafanikio hayo.

Kadhalika, taarifa inaonesha kupungua kwa matukio ya ajali za barabarani yaliyoripotiwa katika kipindi cha Julai – Disemba, kutoka ajali 85 mwaka 2011 hadi ajali 59 mwaka 2012 (yamepungua kwa asilimia 31). Ingawa idadi ya ajali ni ndogo zaidi mwaka jana, ikilinganishwa na mwaka juzi, lakini jumla ya watu kumi na moja walifariki dunia kwa ajali mwaka jana ikilinganishwa na wanne tu mwaka 2011 (vifo vimeongezeka mara tatu).

Kwa upande wa watu waliojeruhiwa kutokana na ajali za barabarani kwenye mkoa huu, taarifa imeonesha kuwa katika mwaka 2012 jumla ya watu 61 walijeruhiwa na katika mwaka 2011 jumla ya watu 44 ndio waliojeruhiwa (ongezeko la asilimia 39). Katika hali kama hii tutaona kuwa tunaweza kuwa na idadi ndogo ya ajali za barabarani lakini zikaleta athari kubwa kwa wananchi.

Natoa wito kwa uongozi wa Mkoa kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama, Jeshi la Polisi pamoja na wananchi kuzingatia sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa madereva hawaendi mwendo wa kasi barabarani, madereva na vyombo vyao vinaangaliwa na pia kuepuka kujaza abiria wengi katika gari zao na wengine kuwaweka kwenye sehemu zisizostahiki.

2.2 **Kilimo:**

Nimeridhishwa na jitihada za wananchi wa Mkoa huu katika kilimo cha mazao mbali mbali kama taarifa ilivyoeleza. Nimeridhishwa vile vile na taarifa ya maandalizi ya kilimo na hasa kilimo cha mpunga ambapo eka 121.75 zimelimwa na kupandwa na eka 119 (asilimia 98) ndizo zilizoota kwa mabonde ya Wilaya ya Kusini. Kwenye mabonde ya mpunga ya Wilaya ya Kati mmeweza kulima eka

3,240.50 na kupanda eka 2,681.75 ambapo eka 1,055.52 zimeota (asilimia 33 ya eka zilizolimwa).

Shughuli hizi za ukulima wa mpunga pamoja na ukulima wa mazao mengine ya chakula na mboga ambazo zimeoneshwa kwenye taarifa zinatia moyo sana. Vile vile, nimevutiwa na jitihada zilizoelezwa kuhusu upatikanaji wa miche ya aina mbali mbali ikiwemo ya matunda, misitu na mazao ya biashara yaani mikarafuu na minazi katika vitalu vinavyomilikiwa na Serikali na vile vya watu binafsi.

Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada za wakulima na kuzifanyiakazi changamoto zilizopo na kuwapatia ruzuku ya pembejeo za kilimo na huduma za matrekta kama tulivyoahidi.

2.3 **Utalii:**

Taarifa imeelezea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya utalii na suala zima la Utalii kwa Wote ambapo Mkoa una hoteli na nyumba za kulaza wageni zipatazo 105. Jumla ya hoteli 37 zipo katika hadhi ya kuanzia nyota moja hadi tano na pia, mnatarajia kupata hoteli nyengine mpya hivi karibuni. Mmeeleza kuwa licha ya kuwepo kwa chagamoto katika uendeshaji wa shughuli za utalii Mkoani kwenu, lakini vijana wengi wamepata ajira katika sekta hii. Kauli yenu ya kuwa mmeanza kutekeleza dhana ya Utalii kwa Wote kwa kuunda Kamati inanipa moyo na nategemea kuwa wananchi watazidi kuhamasika na kushiriki kikamilifu katika sekta hii ili waweze kunufaika zaidi. Hivyo itachangia sana kufanikiwa kwa azma ya Serikali ya kuufanya utalii kuchangia katika jitihada za kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

Natoa wito kwa viongozi wa Mkoa huu kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na vyombo vya ulinzi na usalama, wenye mahoteli na nyumba za kulala wageni pamoja na wananchi kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote zinazokwamisha ufanisi katika kuimarisha utalii. Pamoja na taarifa ya kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama katika Mkoa wenu, bado kuna taarifa za baadhi ya matukio ya uporaji wa watalii kwenye Mkoa wenu. Hivyo Mkoa lazima uhakikishe kuwepo kwa jitihada za makusudi za kukabiliana na matukio hayo kwa wageni kwani

yataushushia hadhi Mkoa wenu na nchi yetu yenye sifa kubwa ya amani na usalama.

2.4 **Ushirika:**

Muamko mkubwa walionao wananchi wa Mkoa huu katika kuendeleza shughuli za ushirika ambazo zina mchango mkubwa katika kuwasaidia wananchi kujiongezea kipato na kupunguza umasikini ni mzuri. Taarifa imeonesha idadi ya vikundi vya ushirika vipatavyo 300 vikiwemo vya kilimo, SACCOS, na vyama vyenye kujishughulisha na kazi mbali mbali.

Serikali nayo inaziunga mkono jitihada za wananchi kwa kuvipatia vikundi hivi mafunzo ya kuwajengea uwezo, kuvifanyia ukaguzi na kuvipatia mitaji. Mfano mzuri ni kiasi cha fedha taslim zipatazo Tshs. 68,900,000 ambazo zimetolewa kwa vikundi 47 kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Nawasihi wananchi waendelee na vikundi vya ushirika kwa shughuli mbali mbali kulingana na mazingira na mahitaji ya kiuchumi na kijamii. Uongozi wa Mkoa na Wilaya zote muwe karibu na vikundi hivi pamoja na kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kukabiliana na changamoto zilizopo ili azma ya Serikali ya kuanzisha wizara hii iweze kufikiwa.

2.5 **Elimu:**

Sote tunafahamu umuhimu wa elimu kwa mwanadamu hasa watoto wetu. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, tokea awamu ya kwanza imekuwa ikichukuwa juhudi mbali mbali kuhakikisha kuwa watoto wa nchi hii wanapata fursa ya kupata haki yao ya elimu mjini na vijijini. Ndiyo maana kila siku Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya sekta hii na kuongeza nyenzo mbali mbali sambamba na kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa katika skuli zetu. Tunaendelea na ujenzi wa skuli mpya, kuzifanyia matengenezo makubwa baadhi ya skuli zilizopo pamoja na kuyaimarisha mazingira ya elimu kwa jumla. Lengo la jitihada zote ni kuwapa watoto wetu fursa ya elimu iliyo bora itakayowafaa wao na familia zao, jamii inayozunguka na nchi yetu nzima kwa jumla.

Taarifa ya sekta ya elimu inaonesha kuwa tumeweza kuwapatia fursa ya kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2013 watoto wote 3,251 walioandikishwa na katika skuli nyingi za mkoa huu, hasa katika Wilaya ya Kusini, wanafunzi wanakwenda

skuli kwa mkondo mmoja tu (asubuhi), na vile vile Mkoa umepata nyongeza ya walimu 20 kati ya mwezi Julai hadi Disemba 2012. Hata hivyo, mafanikio haya yametiwa doa na hali ya utoro wa wanafunzi ambao ni asilimia 6 kwa skuli za msingi na asilimia 7 kwa skuli za sekondari.

Kadhalika, licha ya kuonesha kupungua kwa idadi ya wanafunzi waliopewa ujauzito na waliofunga ndoa kutoka kesi 71 za mwaka 2011 hadi kesi 20 kwa mwaka 2012 (zimepungua kwa asilimia 72), hali inaonesha kuwa mkoa bado una kazi kubwa ya kufanya kwa kuandaa mkakati mahsusi wa kukabiliana na tatizo hili pamoja na utoro wa wanafunzi. Kwa bahati mbaya taarifa yenu haikuonesha mikakati yenu ya kukabiliana na changamoto hizi.

Taarifa ya matokeo ya mitihani ya Taifa ya kidato cha nne mwaka 2012 kwa wanafunzi walioko skuli na waliofanya mitihani ya faragha, haitoi matumaini mazuri. Taarifa inaonesha kiwango cha kupasi kwa watahiniwa wa skuli ni asilimia 25.77 kwa watahiniwa 1261 waliofanya mitihani. Kiwango cha kupasi kwa wanafunzi wa faragha ni asilimia 9.40 kati ya watahiniwa 1527 (wa faragha) waliofanya mitihani katika mwaka huu.

Uongozi wa Mkoa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na wazazi lazima muwe pamoja kutafuta dawa ya kuondoa tatizo hili. Ni dhahiri kuwa kuna tatizo ambalo linapaswa lifahamike na lipatiwe dawa. Aidha, uongozi wa Mkoa ushirikiane na viongozi wa Wilaya, majimbo na wananchi kuanzisha vituo vya kazi za amali ili kuwapa fursa wale vijana ambao hawakupata sifa za kuendelea na masomo kama inavyofanyika katika baadhi ya maeneo hapa Zanzibar.

2.6 **Mengineyo Kuhusiana na Taarifa:**

Taarifa yenu haikueleza chochote kuhusiana na jitihada za Mkoa kuhusiana na mapambano dhidi ya matumizi ya dawa ya kulevya. Kadhalika, chagamoto mbali mbali nilizozitaja hazikuwekewa mikakati ya kuzitatua. Jengine ni kuwa, Kiambatisho cha mwisho, mmekiita Ahadi za Mheshimiwa Rais. Lakini kilichoandikwa kwenye Jadweli hii ni maagizo mbali mbali yaliyotolewa na kutakiwa yatekelezwe. Kwa mafano kupatiwa makobe wawili (jike na dume) kwa wakulima wa Jozani (UWEMAJO) hii siyo ahadi ya Mheshimiwa Rais ila ni agizo kwa hivyo taarifa itenganishe maagizo mbali na ahadi zinazotolewa mbali.

Baada ya maelezo hayo ya jumla kuhusiana na taarifa yenu ambayo kama nilivyotangulia kusema imetayarishwa vizuri na kusomwa vizuri, sasa tuje kwenye ziara tuliyoifanya tarehe 9 kwa Wilaya ya Kati na tarehe 11 yaani leo kwa Wilaya ya Kusini.

## 3.0 ZIARA:

Siku ya tarehe 9 Machi, 2013 ni siku ya Wilaya ya Kati ambapo baada ya kupokea taarifa ya Mkoa pale Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tunguu, nilikagua mradi wa maji Machui na baadae kukagua maendeleo ya ujenzi wa nyumba za maendeleo Mpapa. Wakati wa jioni nilifungua mradi wa maji safi na salama katika kijiji cha Chwaka.

Hivi leo ni siku ya pili ya ziara yetu katika Mkoa huu, tumeanza kwa kuonana na wakulima wa mpunga wa bonde la Muyuni, Kajengwa ambapo tulikagua kituo cha afya na kupokea taarifa na hatimaye tulifika Jambiani kwenye ujenzi wa Ofisi ya mradi wa mazingira wa Tuishi.

### 3.1 Huduma ya Maji Safi na Salama:

Katika siku ya kwanza ya ziara, nilipata fursa ya kukagua maendeleo ya Mradi wa Maji Machui, mradi ambao ni mmoja kati ya miradi ya maji safi na mazingira inayotekelezwa kwa ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Makaazi (UN-Habitat) na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi wote kwa jumla unagharimu jumla ya T.Shs. bilioni 67.73 na utasaidia sana kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira kwa skuli zipatazo 81 za Unguja na Pemba.

Katika eneo la Machui nimeelezwa kuwa mradi huo utahusisha uchimbaji wa visima vikubwa vitatu (3) vya kuzalishia maji na visima vine (4) vidogo vya kufanyia uchunguzi wa maji pamoja na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 13.4. Kwa kweli nimeridhika na hatua ya miradi hiyo ambapo itakapomalizika, itasaidia sana kupatikana kwa huduma za maji safi na salama kwa wananchi wapato 31,000 wa shehia ya Machui, Koani, Ubago, Kidimni na baadhi ya maeneo ya shehia ya Kiboje, Mgenihaji, Miwani, Mwera Pongwe na maeneo yaliopo jirani.

Kadhalika, wakati wa jioni ya siku ya tarehe 9 nilizindua mradi wa maji safi na salama kwa wananchi wa kijiji cha Chwaka mradi ambao umegharimu kiasi cha T.Shs. 330 milioni. Mradi huu ambao ni ukombozi mkubwa wa kupata huduma ya maji safi kwa wananchi wa Chwaka, umetokana na ushirikiano mzuri kati ya wananchi na viongozi wa Jimbo la Chwaka na Serikali.

Napenda niwapongeze tena wananchi wa Chwaka kwa mafanikio hayo. Aidha, natumia fursa hii kuwasihi wananchi waendelee kuwa na subira na kujua kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa ili kuhakikisha kuwa huduma za maji safi inawafikia wananchi wote mijini na mashamba. Kadhalika, wananchi waendelee kuvihifadhi vianzio vya maji na kuacha kuiharibu miundombinu ya maji kwa kutoyatoboa mabomba na kuunga maji bila ya kuzingatia utaratibu.

3.2 **Nyumba za Maendeleo:**

Katika siku yangu ya kwanza ya ziara nilikwenda kukagua hatua za ujenzi wa nyumba za maendeleo katika kijiji cha Mpapa. Nimeridhishwa na hatua ya ujenzi ilipofikia. Mategemeo yangu ni kuwa ujenzi huu utaendelezwa na kukamilika baada ya muda si mrefu ujao.

Hatua ya kuendeleza ujenzi wa nyumba za maendeleo za Mpapa ni kutekeleza azma ya mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume ya kuwajengea makaazi bora wananchi wa Zanzibar ikiwa ni moja ya matunda ya Mapinduzi. Mkoa wa Kusini umebahatika kuwa na nyumba hizi za maendeleo za ghorofa katika kijiji cha Mpapa na kijiji cha Makunduchi.

Nawasihi wale watakaopata fursa ya kuzitumia nyumba hizi ambazo ni chache na wale ambao tayari wameishi kwenye nyumba za maendeleo wawe watunzaji wazuri ili lengo la kuishi katika mazingira yaliyo bora zaidi lipatikane. Wakaazi wajitahidi na usafi hasa wa makaro na taka pamoja na kuacha kufanya shughuli zitakazodhoofisha ubora wa nyumba hizi. Tuzingatie usemi maarufu wa kitunze, kidumu.

3.3 **Kilimo:**

Leo, katika ziara yangu ya Wilaya ya Kusini nimekutana na wakulima wa mpunga katika kijiji cha Muyuni. Tofauti na mara ya mwisho tulipokutana wakanieleza

mafanikio yao ya kilimo cha mpunga na kuomba niwapatie kinu cha mpunga. Mara hii ndugu zangu hawa walinieleza mtihani walioupata kwa mpunga wao kwa asilimia kubwa kukauka na kuwakatisha tamaa.

Kwa mara nyengine napenda kuwapa pole wakulima wetu kutokana na tatizo la kuharibikiwa katika kilimo chao. Nawasihi wasikate tamaa ila waendelee kufuata utaalamu na ushauri unaotolewa na mabwana-shamba na mabibi-shamba wetu. Maelekezo yao yakiwemo utumiaji wa mbegu bora, kutumia dawa ya kuulia magugu na kutia mbolea kwa kuzingatia kwa wakati na viwango vinavyofaa ni muhimu yakafuatwa. Wakulima hawanabudi kuondokana na kilimo cha mazowea hasa wakati huu ambao shughuli za kilimo zinapaswa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi. Serikali inaendelea na jitihada za kuwasaidia wakulima ili shughuli hii muhimu iwe na tija zaidi.

3.4 **Huduma za Afya:**

Nimeridhishwa na jitihada zilizoanzishwa na wananchi wa shehia ya Kajengwa kupitia kamati yao ya maendeleo kwa kushirikiana na viongozi wao, wahisani na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa kuanzisha ujenzi wa kituo cha afya. Sote tunaelewa kuwa hakuna mbadala wa afya.

Napenda kuwapongeza sana wananchi hawa kwa uamuzi wao wa kuanzisha ujenzi wa kituo hiki tangu mwaka 1992 ambacho kitawasaidia kupata huduma kwa karibu kwa maradhi ya kawaida badala ya kwenda kwenye hospitali ya “Cottage” ya Makunduchi kwa kila tatizo ambayo ni masafa kidogo. Nina imani kubwa kuwa kutokana na hatua iliyokwishafikiwa niliyoiona, ujenzi wa kituo hicho utakamilika kwa haraka na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya ya Kusini zishirikiane na Wizara ya Afya kuona kuwa nguvu hizi za wananchi zinaendelea kuungwa mkono. Aidha, changamoto nyengine zikiwemo tatizo la maji na njia ya kufikia kituo nazo zitashughulikiwa.

3.5 **Suala la Mazingira:**

Nilipata fursa ya kukagua hatua za ujenzi wa Jumuiya ya Mazingira iliyopewa jina la Tuishi katika kijiji cha Jambiani. Niliridhishwa na jitihada za wananchi kuamua kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira, kupambana na malaria na pia

kujihusisha na mradi wa kuwajengea vyoo wananchi hasa wale wenye uwezo mdogo ambapo vyoo 327 vilijengwa na vyengine 52 vilifanyiwa matengenezo. Pia, wamejihusisha na utoaji wa mafunzo dhidi ya maambukizo ya maradhi ya UKIMWI. Ni jambo zuri kuwa Jumuiya ya Tuishi imeona haja ya kuimarisha uchumi kwa wanachama wake kuendeleza miradi ya uvuvi na shughuli za ufugaji wa kuku na mbuzi.

Natoa wito kwa uongozi na wanachama wa Jumuiya hii kutovunjika moyo kutokana na changamoto zinazoikabili katika utekekezaji wa shughuli na malengo yake. Serikali itaendelea kuziunga mkono jitihada za vikundi kama hivi ambavyo hufanya kazi zake kwa kujitolea zaidi kwa kuwa karibu navyo na kushirikiana navyo kwa kila hali katika kukabiliana na changamoto zilizopo.

3.6 **Kuhifadhi na Kuyatumia vizuri Maeneo ya Uwandani:**

Wakati nikiwa katika mkoa huu, nimekuwa nikichunguza kwa makini ukubwa wa ardhi tuliyonayo ambayo haijatumika pamoja na matumizi yake. Napata faraja kubwa, kuona kuwa mkoa huu bado una maeneo mengi ambayo hayajatumika ingawaje ni maeneo ya ardhi ya maweni. Imani yangu ni kuwa tunaweza kuyatumia vizuri kwa mahitaji yetu hivi sasa na kuyahifadhi kama ni amana tuliyopewa kwa ajili ya vizazi vijavyo tukitia maanani kwamba kutokana na maendeleo ya teknolojia, ardhi ya uwandani inaweza kutumika kwa shughuli nyingi zikiwemo za viwanda, kilimo na makaazi ya watu.

Wakati Serikali imeanza mikakati kutekeleza mipango miji na tukiwa tumekabiliwa na tatizo la udogo wa ardhi, nachukua fursa hii kuuagiza uongozi wa Mkoa huu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Serikali za Mitaa na kuyashughulikia ipasavyo maeneo yote ya uwanda ambayo ni mali ya Serikali na kuyazuia na uvamizi, uuzaji usio wa lazima nakufikiria matumizi bora ya hapo baadae. Aidha, natoa wito kwa wananchi kufuata taratibu zilizopo ikiwa wanataka kuyatumia maeneo hayo kwa shughuli za kilimo na nyengine.

4.0 **Mambo Maalum:**

Kabla ya kumaliza nasaha zangu napenda niseme mambo yafuatayo ambayo uongozi wa Mkoa, watendaji, taasisi na wananchi wa mkoa huu nawasihi wayasimamie kwa ufanisi zaidi.

1. Nasisitiza tena haja ya viongozi wa taasisi mbali mbali zinazohusika katika miradi tunayoitembelea kuwepo katika ziara hizi ili kuleta urahisi wa utekelezaji wa maagizo yanayotolewa katika ziara zetu.
2. Mkoa ushirikiane na Wizara ya Kilimo na Maliasili na Jumuiya za Wananchi zinazopakana na Hifadhi ya Msitu wa Jozani katika kuandaa mikakati na kusimamia ili kuondokana na tatizo la kutokea kwa moto wa mara kwa mara katika hifadhi hiyo muhimu kwa nchi yetu.
3. Mkoa ushirikiane na viongozi wa wilaya, majimbo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufungua vituo vya kazi mbali mbali za amali kwa ajili ya kuwapatia mafunzo vijana wanaokosa fursa ya kuendelea na masomo yao ya skuli.
4. Suala la utoro wa wanafunzi lililofikia asilimia 6 kwa skuli za Msingi na asilimia 7 kwa skuli za Sekondari, Mkoa ulisimamie na katika kipindi cha ziara ijayo, itolewe taarifa kwamba limemalizika.
5. Tatizo la wanafunzi wanaopata ujauzito nalo lishughulikiwe ili asilimia 28 iliyosalia nayo izidi kupungua angalau kwa nusu katika kipindi cha miezi 9 ijayo.
6. Naelewa kwamba bado ipo migogoro ya ardhi ndani ya Mkoa wenu. Ni vyema mkaendelea kuipatia ufumbuzi kwa kuutumia uzoefu mlioupata wa kutatua mgogoro wa Mchangamle.

   Matatizo ya Wilaya zenu na Mkoa wenu muyaamue wenyewe msiwaachie watu wengine wakuamulieni; kwani mnao uwezo wa kuamua.
7. Viongozi ni vyema wawe karibu na wananchi wakati wote ili kuwasaidia katika shughuli zao za maendeleo. Tusiwaache wananchi wakasikitika mpaka kwa yale mambo ambayo tunaweza kuyapatia ufumbuzi.
8. Nyumba za Mpapa baada ya kukamilika ujenzi, ugawaji wake uzingatie mahitaji ya watu wanaoishi Mpapa wenye shida ya makaazi.

9. Natoa wito kwa viongozi na wananchi wote kuwa na moyo wa kuunga mkono kwa hali na mali shughuli mbali mbali za maendeleo zinazoanzishwa kwa njia ya kujitolea.

5.0 **M W I S H O:**

Napenda kukamilisha hotuba yangu ya majumuisho kwa kuwashukuru tena wananchi wa Mkoa wa Kusini kwa ushirikiano wenu katika ziara yangu ya siku mbili mimi na wenzangu. Natoa shukrani za dhati kwa zawadi nyingi na nzuri mlizonipatia. Hii ni hidaya muhimu kwangu kwa kunionesha mapenzi makubwa. Inshallah tuendelee kuwa pamoja katika masuala mbali mbali ya maendeleo ya nchi yetu kwa kutilia maanani haja ya kushirikiana katika masuala yetu yote kwa faida ya nchi yetu.

Nakushukuruni tena kwa ushirikiano na asanteni sana kwa kunisikiliza